# Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto

Doroth F. Mosha


## Ikisiri

Makala haya yanahusu athari za mgawanyo tofauti wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto kwa watoto. Makala yameangazia zaidi kubaini majukumu ya kijinsia na namna yalivyogawanywa na kisha kuchambua athari zinazoweza kujitokeza kwa watoto kutokana na mgawanyo huo. Kwa mujibu wa mgawanyo huo tuna maoni kwamba kuna athari chanya na hasi zinazojitokeza kwa watoto wanaozitumia nyimbo hizi. Kwa kuzingatia uwiano wa mgawanyo huo kwa watoto, watoto wa kike huathiriwa zaidi kwa upande hasi kuliko watoto wa kiume. Fasihi ya watoto kwa ujumla na nyimbo za watoto zikiwamo kwa upande mmoja na suala la jinsia kwa upande mwingine ni mambo yanayohitaji utafiti zaidi kutokana na umuhimu wake katika kuwaandaa watoto ili wawe na msingi thabiti wa kutekeleza majukumu mbalimbali kulingana na uwezo wa mtoto na sio kwa kuzingatia jinsi ya mtoto. Carlson na wenzake (2004) wana hoja kwamba ubaguzi wa majukumu wa muda mrefu unawaathiri sana watoto katika hatua ya ujana. Vilevile, huo ni umri ambao msingi wa majukumu ya kijinsia hujengwa na kuimarika. Data za makala haya zilikusanywa kutoka katika shule za awali na shule za msingi hadi darasa la nne katika jiji la Dar es Salaam. Mbinu ya ukusanyaji wa data iliyotumika ni ushuhudiaji wa kushiriki.


## 1.0 Utangulizi

Nyimbo za watoto[1] ni kipera cha ushairi - simulizi na ni miongoni mwa kazi za fasihi ya watoto na fasihi kwa ujumla ambacho hupendwa na hutumiwa sana na watoto. Watoto hupenda sana nyimbo hususani sauti za wahusika katika nyimbo hizo (Weche, 2000). Nyimbo za watoto ni sehemu muhimu ya

[1] Ndulute (1977) anafasili nyimbo za watoto kuwa ni zile zinazoimbwa na watoto wakiwa shuleni au katika michezo yao ya kila siku. Naye Simiyu (2002) anasema nyimbo za watoto ni aina ya nyimbo ambazo huimbwa au huimbiwa watoto ili washawishike kihisia kufanya jambo fulani kama vile kulala na kunyamaza kulia. Makala yetu yanazingatia fasili ya Ndulute.

utamaduni na malezi kwa watoto na ni miongoni mwa nyenzo zinazomjenga mtoto kitabia na kumwathiri kijinsia. Nyimbo hizi huimbwa katika michezo ya watoto na katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji wa watoto darasani hususani katika shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi. King'ei na Kisovi (2005) wanasema kuwa nyimbo ni kipera kimojawapo cha ushairi ambacho huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watoto na wakati mwingine kwa kupokezana. Zipo nyimbo za watoto ambazo huimbwa na watoto kwa pamoja kama vile nyimbo katika Jedwali 1: Na. 1 *Mapera Mapera*, Na. 2 *Saa Imefika*, *Na.* 3 *Kondakta Dereva*, Na. 5 *Ukuti Ukuti* na nyingine nyingi. Baadhi ya nyimbo huimbwa na watoto kwa kupokezana yaani huwa na kiongozi anayeanza wimbo na kisha watoto wengine huimba baada ya kiongozi, kwa mfano, nyimbo Na. 6 *Kachiri*, Na. 7 *Namsaka Mke Wangu* na kadhalika.

Nyimbo za watoto ni nguzo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji na ndio sababu zinatumiwa na walimu kufundishia masomo mbalimbali katika shule za awali na shule za msingi. Aidha, nyimbo za watoto hutumiwa na wazazi au walezi wakati watoto wanapokuwa nyumbani na pia hutumiwa na watoto katika michezo yao. Nyimbo hizi huelimisha, huburudisha na hutoa maadili yenye lengo la kumpatia mtoto malezi bora. Watoto hufunzwa pia matendo mema na mambo mengine mbalimbali muhimu katika ukuaji wao kama vile upendo, ujasiri, mafanikio, jinsia na hata falsafa ya Kiafrika (Mulokozi, 1975; Msokile, 1981; Ndumbaro, 1993; Mwanzi, 2006; na Omari, 2008). Mafunzo haya huwafikia watoto kupitia wahusika kwa namna wanavyobebeshwa majukumu katika nyimbo hizo.

Ni vema katika makala haya kufafanua dhana ya jinsia ilivyotumika kwa kuwa wakati mwingine huchanganywa katika kuzitafsiri. *Jinsia* ni istilahi inayotumika sambamba na ile ya *uana* (TUKI 2005: 132) ijapokuwa baadhi ya wataalamu kama vile Tuttle (1986) na Ostergaad (1992) wamezitofautisha kwa kusema kuwa *uana* (gender) ni istilahi inayohusu muundo wa jamii husika; namna jamii unavyomchukulia mwanamke na mwanamume na nafasi zao. Wamefasili dhana *jinsia* (*sex*) kuwa ni maumbile ama suala la kibiolojia, yaani mwanamume au mwanamke anajulikana hivyo kutokana na maumbile yake. Mtazamo wao unapingana na ule wa Shirika la WiLDAF (2011: 2) ambalo humaanisha *jinsi*. WiLDAF wanafafanua kuwa *jinsia* ni mahusiano ya kijamii kati ya wanawake na wanaume, namna yalivyojengwa na jamii kutokana na mila, desturi na tamaduni za jamii hiyo. Jinsia huundwa kijamii na kiutamaduni (Lyimo, 2014). Mahusiano ya kijamii ambayo huaminika kuwa ya kweli, yanaanzishwa na jamii kama wazo na baadaye wazo hilo bila kupingwa huimarika na kuwa ndiyo uhalisi wenyewe (Berger na Luckman, 1990).

Mnenuka (2017) anafafanua zaidi kwamba, kile ambacho watu hukichukulia kuwa ni uhalisi kimejengwa na jamii husika. Hivyo basi, istilahi *jinsia* inayomaanisha muundo na mahusiano ya kijamii ambayo yamejengwa na jamii yenyewe ndiyo itakayotumika katika makala haya.

Uchunguzi kuhusu majukumu ya kijinsia[2] katika fasihi ya watoto (nyimbo zikiwapo) ni muhimu kufahamu kwa kuwa changamoto zinazotokana na mgawanyo wa majukumu ya kijinsia huathiri mahusiano ya watoto ya baadaye. Iwapo ujumbe unaowasilishwa na fasihi ya watoto kwa watoto ni tofauti na maadili mahususi wanayofunzwa, huweza kuleta athari kwa upande wa mtoto. Halikadhalika, endapo majukumu ya kijinsia katika fasihi ya mtoto hayaakisi masuala ya wakati uliopo, itachukua muda mrefu kwa masuala hayo kuonekana ya kawaida katika jamii husika. Hivyo, nyimbo za watoto ni miongoni mwa rasilimali ambazo husawiri majukumu ya kijinsia yenye kumfanya mtoto kuiga majukumu ya jinsi yake kupitia wahusika wa nyimbo hizo.

Makala haya yanalenga kueleza athari za mgawanyo wa majukumu ya kijinsia zinazoweza kumpata mtoto anayezitumia nyimbo hizi za watoto. Data za makala haya (nyimbo za watoto) zilitoka kwa wanafunzi wa madarasa ya awali hadi darasa la nne katika shule za msingi katika mkoa wa Dar es Salaam. Shule zilizoshiriki ni Mji Mpya, Makumbusho, Mchikichini na Bunju A. Shule hizi ziliteuliwa kinasibu kutoka katika kata zilizopatikana kwa kutumia sampuli taratibishi kutoka katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke. Mtafiti aliwaomba watoto wamwimbie nyimbo wanazozijua na kuzirekodi. Aidha, kwa kuwa hawakuwa na muda wa kuimba nyimbo nyingi, mtafiti aliwaomba waziandike nyimbo ambazo hawakupata wasaa wa kuziimba na kisha kuzikusanya. Mjadala wa makala ni wa kimaelezo na umejikita kuchambua namna nyimbo hizo zinavyoweza kuleta athari katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kijinsia kwa watoto wanaoziimba.

Makala inaongozwa na Nadharia ya Skima ya Kijinsia[3] ambayo mwasisi wake ni Bem (1981), na kuendelezwa na Martin na Halverson (1983).

---

[2] Utafiti huu umezingatia fasili iliyotolewa na Tanganyika Law Society (2016) wanaosema, majukumu ya kijinsia ni kazi mbalimbali, wajibu na matarajio ambayo jamii imetafsiri na kupanga kufanywa na wanaume na wanawake, wasichana na wavulana na watoto wa kike na wa kiume. TLS wanafafanua zaidi kuwa kazi hizi sio za kibiolojia kwa hiyo zinaweza kubadilika kufuatana na wakati na mazingira yaliyopo. Wajibu uliopangwa kufuatana na jinsi ni utaratibu wa jamii na umekuwa ukibadilika kulingana na wakati.

[3] 'Skima' ni istilahi iliyotafsiriwa kutoka neno la Kiingereza *Schema* ikiwa na maana ya muundo tambuzi, yaani mtandao wa miungano unaoratibu na kuongoza utambuzi binafsi. (Neisser, 1976). Huu pia huitwa muundo ngojezi ambao huingiliana na taarifa ingizi (*incoming information*) kutoka katika jamii husika ili kupata uelewa na maarifa kuhusu jambo fulani.

Nadharia hiyo inafafanua kuwa watoto huanza polepole kujijengea utambulisho wa kijinsia kadiri wanavyojifunza mfumo wa mawazo na yale yanayohusiana na utamaduni wao. Watoto hawa hushuhudia mambo mbalimbali yanayofanywa na watu wengine na kujifunza kutokana na wanachokifanya hasa majukumu anuwai yanayotokana na mazingira na utamaduni ambayo yanafanywa na wanaume na wanawake. Mtazamo huu unatumika kumwandaa na kumwelekeza mtoto tabia zinazoendana na mila na desturi na matarajio yanayohusiana na jinsi ya mtoto. Martin na Halverson (1983) wanaeleza kuwa watoto hutafuta ukweli wa taarifa zinazohusu majukumu, tabia na sifa bainishi za kijinsia zinazofaa. Kwa hali hii, watoto huchukua kila wanachokishuhudia kinachomhusu mwanamume na mwanamke na kuvipangilia katika mtazamo wa kijinsia.

Wanafafanua zaidi kuwa, mtoto hushuhudia kuwa mama ndiye anayefanya kazi za nyumbani ikiwa ni pamoja na kuwaandaa tayari kwa kwenda shuleni. Baba huwa anakwenda kazini, hufanya kazi chache sana awapo nyumbani na ndiye mtoa adhabu. Kwa kushuhudia hayo, mtoto anakuza mtazamo wake kuwa wanawake wameumbwa kwa ajili ya kufanya kazi za nyumbani ilhali wanaume wapo kwa ajili ya kutoa adhabu na mahitaji ya familia. Mtazamo huo ndio unaojenga na kukuza ubaguzi wa majukumu ya kijinsia kama asemavyo Bem (1981). Mwasisi huyu anabainisha kuwa Nadharia ya Skima ya Kijinsia ni namna ya kufafanua ubaguzi wa kijinsia ambao wanajamii wengi wanapambana kuukwepa. Nadharia ya Skima ya Kijinsia imetuwezesha kufafanua majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto, yaani watoto hujifunza majukumu yanayoendana na jinsi zao kupitia nyimbo zao na hatimaye ujifunzaji huo huwa na athari katika maisha yao. Ikumbukwe kwamba ujifunzaji huu kwa watoto si wa kukusudia.

Makala haya yana sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unazungumzia kwa ufupi kuhusu nyimbo za watoto na muhtasari wa nadharia inayoongoza makala haya. Sehemu ya pili inahusu utendaji katika nyimbo za watoto kwa kuwa watoto huigiza kwa matendo baadhi ya majukumu yanayoendana na jinsi zao wakati wanapoimba. Sehemu ya tatu inajikita kueleza mgawanyo wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto. Sehemu ya nne ni mjadala kuhusu athari za mgawanyo wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto kwa watoto na sehemu ya tano ni hitimisho la utafiti wa makala haya.

## 2.0 Utendaji katika Nyimbo za Watoto

Uwasilishaji wa nyimbo za watoto hufanyika kwa namna mbili: uwasilishaji kwa njia ya masimulizi ya mdomo (Finnegan, 1992) na uwasilishaji kwa njia ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kwa mfano, magazeti, redio, luninga na video (Mrikaria, 2012 na Ussi, 2015). Uwasilishaji wa nyimbo za watoto

tunaozungumzia katika makala haya ni ule wa masimulizi ya mdomo ukihusisha viungo vya mwili na kufanya matendo halisi yanayoakisi uhalisi wa maisha ya jamii. Nyimbo za watoto huwasilishwa nje ya nyumba wakati wa jioni watoto wanapokuwa wamerudi shuleni, sehemu yoyote yenye eneo la kutosha kucheza kwa uhuru, darasani (wakati wa kujifunza somo la hisabati na masomo mengine), viwanja vya shule wakati wa mapumziko na ndani ya nyumba kutegemeana na mada, idadi ya watoto na majira ya mwaka (Omari, 2008). Aidha, Omari anafafanua kuwa wakati wa likizo na mwisho wa juma nyimbo za watoto huimbwa wakati wowote.

Mara nyingi nyimbo za watoto huambatana na michezo yao. Watoto wanapoimba huwa na matendo, kwa mfano kukimbia, kujificha, kupiga makofi, kushika/kukata kiuno, kurukaruka, kukaa, kuunda duara, kushikana mikono na matendo mengine mengi kutegemeana na aina ya wimbo husika. Mtoto kila mara anapenda aushughulishe mwili wake (Omari, 2008).

Ni dhahiri kwamba watoto wanapoimba, huigiza kile kinachoimbwa kulingana na aina ya mhusika wa wimbo huo. Katika wimbo Na. 7 *Namsaka Mke Wangu* mtoto wa kiume huchukua nafasi na jukumu la baba la kumtafuta mkewe huku akiwa amebeba bakora, mwenye uso unaoonesha hasira na akitembea kwa ubabe. Mtoto wa kike huvaa nafasi ya mke na kujificha katikati ya duara la watoto wenzake akiwa na hofu, mnyonge na asiyejiamini kwa kile anachokifanya. Halikadhalika, katika wimbo Na. 6 *Kachiri Kachiri* mtoto wa kike huigiza kama mke akielezea kuhusu safari ya mumewe. Hakika baadhi ya nyimbo za watoto huambatana na watoto kuiga majukumu ya kijinsia kwa mfano kupika, kufua, kuchota maji, kufua na majukumu mengineyo. Uigizaji huu unatokana na kile walichokishuhudia kikifanywa na wahusika wanaume na wanawake katika maisha halisi na katika nyimbo zao. Hivyo, watunzi wa nyimbo za watoto nao hugawanya majukumu ya kijinsia kwa namna yanavyofanyika katika jamii husika na kama ambavyo Nadharia ya Skima ya Kijinsia inavyofafanua.

## 3.0 Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto

Katika mazingira ya jamii yoyote ile, mtoto hutambua majukumu yanayoendana na jinsi yake baada ya kushuhudia na kuiga kwa vitendo hali halisi ya yale yanayofanywa na wanaume na wanawake katika mazingira anamoishi. Nadharia ya Skima ya Kijinsia ina hoja kuwa watoto hushuhudia mambo mbalimbali yanayofanywa na watu wengine na hujifunza kutokana na wanachokifanya hasa majukumu anuwai yanayotokana na mazingira na utamaduni ambayo yanafanywa na wanaume na wanawake. Kwa hiyo, nyimbo za watoto zimeakisi majukumu anuwai yanayofanywa na mwanamume na mwanamke yakiwa yamechotwa katika jamii mbalimbali. Majukumu ni kiunzi muhimu sana katika jamii yoyote ile yenye nia ya kujiletea maendeleo yake.

Majukumu yanaweka wazi masuala ya kijinsia kwa namna majukumu hayo yanavyogawanywa na wanajamii. Mgawanyo huo wa majukumu huweza kufanyika kwa urazini au bila urazini wowote (Lyimo, 2014).

Nyimbo za watoto ni kipera kilichobeba suala la jinsia kwa namna majukumu yalivyogawanywa kupitia wahusika wa nyimbo hizo. Nyimbo za watoto zinatumia wahusika watu, nafsi (wasemaji/wasimulizi), vitu, wanyama na mimea; wahusika watu huwa na matendo yenye kusawiri suala la ujinsia. Kila mhusika hupewa jukumu kulingana na mtazamo/itikadi ama falsafa ya mtunzi, uzoefu wake, tukio analoliandikia, mazingira alimolelewa, historia ya jamii anayoiandikia na utamaduni wa jamii husika. Nadharia ya Skima ya Kijinsia inasisitiza kwamba jamii ndiyo inayoamua matarajio na wajibu wa mwanamume na mwanamke, nini kifanywe na mwanamume na nini kifanywe na mwanamke ikiongozwa na utamaduni, miiko na kaida zake mbalimbali. Watunzi wameteua wahusika wanaume na wanawake wa rika zote (wazee, wazazi, vijana na watoto) na kuwabebesha majukumu kwa mujibu wa uzingativu wa vipengele tajwa hapo juu.

Watoto wanapoimba nyimbo hizi hupata taarifa ingizi zinazoingiliana na utambuzi wao na kujinasibisha na wahusika wanaoendana na jinsi zao. Mtoto wa kiume huiga majukumu yanayotekelezwa na mwanamume na mtoto wa kike huiga yale yanayotekelezwa na mwanamke. Kwa mtazamo huo tuchunguze namna watunzi wa nyimbo za watoto walivyogawa majukumu mbalimbali kwa mujibu wa jinsi ya mhusika.

**3.1 Mgawanyo wa Majukumu ya Mwanamume na Mwanamke**

Nyimbo za watoto zimedhihirisha kuwapo kwa majukumu ambayo jamii huchukulia kuwa ni ya mwanamume na kwamba mwanamke hawezi kuyafanya na kinyume chake pia. Inapotokea mwanamume kufanya majukumu fulani yanayosadikiwa kuwa ni ya mwanamke na mwanamke vivyo hivyo, jamii hushangaa na kumwona wa kipekee na tofauti sana. Mtazamo huu hutofautiana baina ya jamii moja na jamii nyingine kwa kuwa kila jamii ina utaratibu wake. Lakini pia familia zinatofautiana katika kutekeleza majukumu anuwai ya mwanamume na mwanamke kutokana na athari za malezi na athari za wale wote wanaozizunguka familia hizo. Muhtasari wa Jedwali Na.1 unabainisha mgawanyo wa majukumu ya wahusika katika nyimbo za watoto:

**Jedwali Na.1: Mgawanyo wa Majukumu Kulingana na Jinsi ya Mhusika**

| **Mifano ya Nyimbo** | **Jukumu** | **Me** | **Ke** | **Me/ Ke** |
|---|---|---|---|---|
| *1. Mapera* 2. *Saa Imefika* 3. *Kondakta Dereva* | Kupika | | ✓ | |
| 4. *Ewe Mama Jeni* | Kutafuta mahitaji ya familia, kufanya kazi za nyumbani, kulea watoto | | ✓ | |
| 5. *Ukuti Ukuti,* | Kutoa adhabu | ✓ | | |
| 6. *Kachiri* | Kutafuta mahitaji ya familia | ✓ | | |
| 7. *Namsaka Mke Wangu*, | Kutoa ruhusa, kutafuta mahitaji ya familia | ✓ | | |
| 8. *Baba na Mama* | Kusoma | ✓ | | |
| 9. *Fursa* | Kusoma | | | ✓ |
| 10. *Wazazi* | Kusoma | ✓ | | |
| 11. *Nampenda*, 12. *Nawapenda* 13. *Nampenda Saidina* | Kutoa mafunzo na nasaha kwa watoto | | ✓ | |
| 14. *Paulo* 15. *Ee Yakobo* | Kusoma | ✓ | | |
| 16. *Mama wa Kambo* 17. *Mbuzi Mbuzi* | Kumiliki mali | ✓ | | |
| 18. *Bibi Kikongwe* | Kukaa nyumbani, kufanya kazi za nyumbani | | ✓ | |
| 19. *Shikamoo Mama* | Kufanya biashara | ✓ | | ✓ |
| 20. *Mama Huyooo* | Kufanya Kazi za shamba | ✓ | | ✓ |
| 21. *Moja Mbili Tatu* | Kuvua samaki | ✓ | | |
| 22. *Ninadunda* | Kugonga/kusaga mawe | ✓ | | |
| 23. *Mwajuma* | Kuchota maji | | ✓ | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2016)

### 3.1.1 Majukumu Tofauti ya Kijinsia ya Mwanamume na Mwanamke

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa watunzi wa nyimbo za watoto hufanya mgawanyo wa majukumu wakiongozwa na kaida za jamii yao. Tafsiri iliyopo miongoni mwa wanajamii ndiyo inayoakisi mgawanyo huu wa majukumu. Tunaona mara kadhaa katika jamii zetu kuwa jukumu la kutoa ruhusa liko mikononi mwa mwanamume/baba. Taz. mfano wa wimbo Na. 7 *Namsaka Mke Wangu*. Mume anauliza “ruhusa kampa nani” kama inavyoonekana hapa chini:

Mfano wa 1:

**7. *Namsaka Mke Wangu***

Mmoja: *Namsaka mke wangu namsaka mke wangu*
Wote: *Hapa hayupo hapa hayupo*
Mmoja: *Kaenda wapi kaenda wapi?*
Wote: *Kaenda kwa msusi kaenda kwa msusi*
Mmoja: *Chanuo kampa nani chanuo kampa nani?*

Wote: *Kampa msusi kampa msusi*
Mmoja: *Ruhusa kampa nani ruhusa kampa nani?*

Mama anapompatia mtoto ruhusa ya kufanya jambo fulani hawezi kuiamini ruhusa hiyo bila ushiriki wa baba. Huenda mtoto amekuwa akishuhudia ruhusa zikitolewa na baba na si mama (Martin na Halverson, 1983). Dhana hii inabaki akilini mwa mtoto kuwa baba ndiye mtoa ruhusa kama tulivyoona katika data. Pia, mazoea haya yamekitwa akilini mwa mama na hivyo mara nyingi hurusha jukumu hili kwa baba. Katika ulimwengu wa mwanadamu yapo mambo yanayohitaji ushiriki wa mume na mke, na pia yapo mambo yasiyokuwa na ulazima wa kusubiri maamuzi ya pamoja, kwa mfano kutoa ruhusa kwa mtoto na mambo mengine ya dharura.

Licha ya jukumu la mwanamume la kutoa ruhusa, yapo majukumu mengine ambayo hufanywa na wanaume katika nyimbo za watoto ambayo yameelezwa kwa muhtasari, kwa mfano, kutafuta mahitaji ya familia katika nyimbo (Na. 6 *Kachiri Kachiri* na Na. 7 *Namsaka Mke Wangu*), kutoa adhabu (Na. 5 *Ukuti Ukuti* na Na. 18 *Bibi Kikongwe*) na kumiliki mali (Na. 17 *Mbuzi Mbuzi*). Katika majukumu haya, si kwamba hakuna wanawake wanaoyafanya bali imezoeleka katika jamii nyingi kuwa yanatekelezwa zaidi na wanaume, na hivyo watunzi wanachota yale waliyoyashuhudia katika jamii zao.

Majukumu kwa upande wa wahusika wanawake katika nyimbo za watoto kwa mujibu wa Jedwali Na. 1 ni pamoja na kupika (Na. 1 *Mapera Mapera*, Na. 2 *Saa Imefika* na Na. 3 *Kondakta Dereva*), kuteka/kuchota maji na kulea watoto (Na. 4 *Ewe Mama Jeni*), kutoa mafunzo na nasaha kwa watoto (Na. 11 *Nampenda* na Na. 12 *Nawapenda*), kufanya biashara (Na. 19 *Shikamoo Mama*) na kilimo (Na. 20 *Mama Huyo*). Majukumu haya hutekelezwa zaidi na wanawake ingawaje baadhi ya wanaume hushiriki katika kufanya baadhi ya kazi hizi.

Kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu katika nyimbo hizi za watoto, ni dhahiri zipo nyimbo za watoto zenye mgawanyo tofauti wa majukumu ya kijinsia ambazo zinatoa taswira hasi na chanya kwa namna majukumu hayo yanavyotekelezwa. Halikadhalika, zipo nyimbo chache zenye mgawanyo sawia wa majukumu ya kijinsia ambazo ni chachu ya kuondoa mipaka katika utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa jinsi ya mhusika. Hivyo, tuone ni kwa namna gani mgawanyo tofauti wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto unavyoleta athari kwa watoto wanaozitumia. Nyimbo za watoto katika Jedwali Na. 1 zimetumika kufafanua athari hizo.

## 4.0 Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto

Nyimbo za watoto kama tulivyoeleza hapo awali ni kipera pendwa kwa watoto. Kipera hiki kinatumiwa na watoto kwa malengo makuu mawili ikiwa ni katika uwanja wa taaluma shuleni na katika michezo yao. Suala la kujifunza majukumu ya kijinsia si kusudio lao bali hujikuta wakiathiriwa kwa yale wanayokutana nayo katika nyimbo hizo. Nadharia ya Skima ya Kijinsia inasisitiza mtoto kujifunza masuala yanayoendana na jinsi yake kwa kushuhudia, kuiga na kusikia yale yanayofanywa na wanaume na wanawake. Watoto wanapoimba nyimbo zao wanajihusisha na wahusika wa nyimbo hizo kwa kuiga na kutenda kulingana na jinsi za wahusika hao. Watoto hufurahia wahusika ambao wako karibu nao (baba, mama, kaka, dada, mjomba, bibi na kadhalika) wanaowaamini, kujitambulisha na kujinasibisha nao na hata kuwaelewa (Huck, 1979). Mtoto wa kike huiga majukumu ya mhusika mwanamke na mtoto wa kiume vivyo hivyo. Imeelezwa hapa chini athari hasi na chanya zinazotokana na mgawanyo tofauti wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo hizo kwa watoto kama ifuatavyo:

## 4.1 Athari Chanya za Mgawanyo Tofauti wa Mujukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto

Zipo athari chanya kwa watoto na jamii kwa ujumla kwa namna ambavyo watunzi wamefanya mgawanyo wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto. Athari hizo zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

### 4.1.1 Huwafunza Watoto Mgawanyo wa Majukumu Kulingana na Jinsi Zao

Mgawanyo wa majukumu katika nyimbo za watoto unawafunza watoto majukumu mbalimbali kwa mujibu wa jinsi zao. Licha ya kwamba watoto kujifunza majukumu yao, huenda mgawanyo huo ukasababisha hali ya usawa kati ya mwanamume na mwanamke au kujiegemeza katika kukandamiza jinsi moja kutokana na utamaduni uliojengeka katika jamii husika na si kwa sababu za kibiolojia. Mgawanyo wa majukumu ambao unahusisha jinsia mara nyingi unamuweka mwanamke katika kiwango cha juu cha kazi zisizo na hadhi (Mackinnon, 1991) yaani kazi zisizokuwa na malipo ambazo zinasawiriwa pia katika nyimbo za watoto. Mara nyingi uimbaji wa nyimbo za watoto huambatana na watoto kuiga na kujinasibisha na matendo ya wahusika wanaofanana nao. Mtoto wa kike huiga matendo ya mhusika mama na matendo ya wahusika wengine wa kike kama vile kupika, kulea watoto, kuosha vyombo na majukumu mengine yanayomhusu mwanamke, na mtoto wa kiume vivyo hivyo huiga na kujinasibisha na majukumu ya mhusika baba na wahusika

wengine wa kiume kwa mfano kwenda kazini, kutoa adhabu, kutoa ruhusa na pia kuiga matendo ya wahusika wengine wa kiume.

Watoto wanapojifunza majukumu katika nyimbo wanazoimba hawana nafasi ya kuhoji namna majukumu hayo yalivyogawanywa bali huzingatia aina ya jukumu na jinsi ambatani. Nyimbo za watoto zimeweka bayana wajibu na majukumu ya mwanamume na yale ya mwanamke. Tutazame mfano wa nyimbo zifuatazo hapa chini:

Mfano wa 2:

| **1. Mapera Mapera** | **2. Saa Imefika** | **3. Kondakta Dereva** |
|---|---|---|
| *Mapera mapera* | *Saa imefika ya kwenda nyumbani* | *Kondakta dereva bibi katikati* |
| *Mama kapika ugali* | *Mama amepika wali na nyama* | *Kondakta dereva bibi katikati* |
| *Na kifaranga cha kuku* | *Kwa kheri, kwa kheri mwalimu* | *Kapika maandazi bila wasiwasi* |
| *Tia hapa tia hapa mmm!* | *Mungu akipenda tutaonana* | *Kondakta dereva bibi katikati* |
| | *Kwa kheri, kwa kheri mwalimu* | *Kapika bagia bila wasiwasi* |
| | *Mungu akipenda tutaonana* | |

Nyimbo hizi za watoto zilizowasilishwa hapo juu zinasisitiza jukumu la mwanamke la kupika. Mama anapika ugali katika data Na. 1, amepika wali na nyama katika data Na. 2 na bibi anaonekana akipika maandazi na bagia katika data Na. 3. Vivyo hivyo, mwanamke ndiye mbebaji wa jukumu la kufanya kazi za nyumbani kama vile malezi ya watoto, kuchota maji na kumhudumia mume. Data Na. 4 inafafanua haya hapa chini:

**4. Ewe Mama Jeni**

*Mama: Abee mume wangu baba Jeni*
*Nimeitika, nilikuwa uani, nikimuogesha mtoto*
*Na jua hili amechoka*
*Baba: Ewe mama Jeni*
*Kumbuka nimerudi saa saba za usiku*
*Hujanitafutia maji ya kuoga*
*Nataka maji*
*Nisisikie ng'eng'eng'e*
*Nataka maji*
*Mama: Nimerudi saa saba hii, mtoto mgongoni, maji mkononi, kuni*
*kichwani na jembe begani*
*Nisamehe mume wangu*
*Mtoto (kike): Basi baba usiwe mkali*
*Mimi mwanao nimetoka shule*

*Nitakutafutia maji kwa haraka*
*Baba: Ewe mtoto mpumbavu*
*Una akili kama za mama yako*
*Uache shule uolewe,*
*Nipate mali nilipe madeni ya pombe*
*Mtoto (kiume): Na mimi baba nataka kusoma*
*Utanilipia karo ya shule?*
*Baba: Sawa wewe mwanangu,*
*Una akili kama baba yako*

Katika wimbo huu pamoja na nyimbo nyingine za watoto za namna hii, mwanamke ana wajibu wa kulea watoto, kuchota maji, kupika, kumhudumia mume na kadhalika. Mtoto wa kike naye hushiriki kazi za nyumbani anapomsihi babake na kumwahidi kumtafutia maji kwa haraka. Mwendelezo wa mgawanyo huu wa majukumu una dalili za kibaguzi na unamkandamiza mtoto wa kike ilhali ukimpendelea mtoto wa kiume. Katika nyimbo hizi, mtoto wa kiume haonekani akishiriki katika majukumu haya. Wanausasaleo wanapinga ubaguzi huu ya kwamba mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke yarejeshe usawa katika utendaji wa kazi mbalimbali. Kama wasemavyo Betty Friedan, Shulamith Firestone na Kate Millet (Tong, 1989) nafasi duni wanayopewa wanawake haitokani na maumbile yao, bali inatokana na jinsi jamii inavyounda dhana ya mwanamke.

Katika kutazama upande wa mwanamume, data Na. 5 *Ukuti Ukuti*, Na. 6 *Kachiri na* Na. 7 *Namsaka Mke Wangu* zina majukumu ya kutoa adhabu, kutafuta mahitaji ya familia na kutoa ruhusa mtawalia. Tuone mifano ya nyimbo hizo:

Mfano wa 3:

**5. *Ukuti Ukuti***
*Ukuti ukuti*
*Wa meme wa meme*
*Mwenzetu mwenzetu*
*Kagongwa kagongwa*
*Na nini na nini*
*Na gari na gari*
*Tumpeleke hosiptalini tusije kuchapwa na baba yake yesa yesa yesa yeee*

**6. *Kachiri***
Mmoja: *Kachiri kachiri*
Wote: *Saga*
Mmoja: *Mume wangu kasafiri*
Wote: *Saga*
Mmoja: *Kaniachia ukili*
Wote: *Saga*
Mmoja: *Upatao pima mbili*
Wote: *Saga*
Mmoja: *Na upande wa hariri*
Wote: *Saga*

**7. *Namsaka Mke Wangu***
Mmoja: *Namsaka mke wangu mansaka mke wangu*
Wote: *Hapa hayupo hapa hayupo*
Mmoja: *Kaenda wapi kaenda wapi?*
Wote: *Kaenda kwa msusi kaenda kwa msusi*
Mmoja: *Chanuo kampa nani chanuo kampa nani?*
Wote: *Kampa msusi kampa msusi*
Mmoja: *Mafuta kampa nani mafuta kampa nani?*
Wote: *Kampa msusi kampa msusi*
Mmoja: *Ruhusa kampa nani?*

Katika data Na. 5, watoto wanashauriana kumpeleka mwenzao hospitalini wakihofia kuchapwa endapo hawatafanya hivyo. Mwanamume anaonekana mtokaji na mtafutaji katika data Na. 6 mke anapoeleza kuwa mumewe kasafiri, na katika data Na. 7 mume anapohangaika kumtafuta mkewe baada ya kurejea nyumbani. Kupitia nyimbo hizi watoto wanajengewa msingi wa kujua majukumu yao kuanzia utotoni.

### 4.1.2 Huonesha Mgawanyo Halisi wa Majukumu Kiwakati

Nyimbo za watoto ni miongoni mwa kazi za kifasihi ambazo maudhui yake hayatokani na utupu (ombwe) bali husawiri matukio ya kijamii ya nyakati mbalimbali. Ni katika maudhui ambamo tunapata utimilifu wa majukumu ya kijinsia ambayo mtunzi huwapachika wahusika wake katika mazingira husika. Mabadiliko ya maudhui ya kazi za kifasihi ni matokeo ya mabadiliko ya kijamii. Hivyo, mabadiliko ya maudhui huenda sambamba na maendeleo na mabadiliko ya mgawanyo wa majukumu katika jamii husika. Mulokozi (1975) na Balisidya (1987) wanakiri kuwapo kwa nyimbo za watoto tangu zamani zinazorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Lakini pia zipo nyimbo za kisasa ambazo ni chachu ya kubadilisha fikra, mitazamo na itikadi za kijamii.

Nyimbo za watoto zimetungwa kwa nyakati mbalimbali zikiwa na mgawanyo wa majukumu unaosawiri nyakati hizo. Nyimbo zilizotungwa miaka ya 1950 na 1970, kwa mfano data za nyimbo Na. 14 *Paulo* na Na. 15 Ee *Yakobo*, zinamsawiri mtoto wa kiume kama ndiye mwenye jukumu na haki ya kupata elimu. Data zinasema:

Mfano wa 6:

| | |
|---|---|
| **14. *Paulo*** | **15. Ee *Yakobo*** |
| *Paulo usije kucheza na mimi una mikono michaafu*<br>*Paulo, Paulo usije kucheza na mimi una mikono michaafu* | *Ee Yakobo, Ee Yakobo, walala walala*<br>*Walala walala amka twende shule*<br>*Amka twende shule*<br>*Haya njoo, haya njoo* |

Katika nyakati hizo mtoto wa kike alisahaulika na kuonekana kwamba jukumu la kupatiwa elimu ni la mtoto wa kiume. Mtazamo huu unapingana na mfano wa 4: wenye data za nyimbo Na. 8, Na. 9 na Na. 10 za nyakati za sasa yaani katika karne hii ya 21 ambapo kupata elimu si jukumu la mtoto wa kiume pekee kama ilivyokuwa hapo awali bali ni wajibu wa watoto wa jinsi zote. Katika nyimbo hizo, wazazi wanahimizwa kutofanya ubaguzi wa elimu kwa watoto kwa kujikita katika kigezo cha jinsi. Pia, data Na. 10 inapinga ubaguzi wa majukumu ya kazi za nyumbani zinazodhaniwa kuwa zinawahusu wanawake na

watoto wa kike pekee kama ambavyo mwanamke ametwikwa jukumu la kufanya kazi zote za nyumbani katika mfano wa 2, data Na. 4. Kwa kuzingatia data hizi chache za nyimbo za watoto ni kwamba, hali halisi ya mgawanyo wa majukumu katika jamii fulani hutokana na uhalisia wa mabadiliko na maendeleo ya jamii husika.

### 4.1.3 Huweka Bayana Mgawanyo wa Majukumu na Utamaduni wa Jamii Husika kwa Watoto

Nyimbo za watoto na suala la jinsia ni dhana sizizoweza kutenganishwa kwa kuwa hutegemeana na kuathiriana katika utendaji kazi. Nyimbo za watoto ni msingi katika ujenzi na ufafanuzi wa mgawanyo wa majukumu ya kijinsia katika jamii kama ambavyo zinafanya katika masuala mengine ya lugha, matabaka, ubaguzi wa rangi, uongozi na mengineyo. Nyimbo za watoto zinatoa uchambuzi halisi wa majukumu ya kijinsia kulingana na utamaduni wa jamii, nyanja za kisiasa na kiuchumi. Watoto wanapoimba nyimbo hizi hupata elimu kuhusu namna mgawanyo wa majukumu unavyotekelezeka katika jamii inayowazunguka na namna utamaduni unavyojipambanua katika mgawanyo huo. Kwa kuwa mgawanyo wa majukumu huundwa na jamii (Burr, 1995), na wakati mwingine kutawaliwa na mitazamo potofu, watoto nao hujengeka ndani ya mitazamo hiyo. Kimsingi tuzingatie tu kwamba utamaduni ni mhimili wa kumfinyanga mtoto kuyajua yale yampasayo kufanya bila kujali kama ni potofu au la.

Kupitia nyimbo, watoto huanza kuelewa majukumu ya mwanamume na ya mwanamke ambayo yamezaliwa kutokana na utamaduni wa jamii hiyo. Mwanamume anapoonekana akitoa adhabu (taz. data Na. 5 *Ukuti Ukuti*), akirithi na kumiliki mali (katika data Na. 16 *Mama wa Kambo na* Na. 17 *Mbuzi*) na mwanamke akionekana katika karakana ya jikoni (data Na. 1, Na 2 na Na. 3), akifanya kazi zote za nyumbani (data Na. 4) ni njia mojawapo ya kuwafanya watoto wafahamu namna utamaduni na mgawanyo wa majukumu ya kijinsia vinavyofungamanishwa. Utamaduni wa jamii za Kiafrika zilizo nyingi unampa mwanamume nafasi ya kwanza katika kumiliki na kurithi mali. Data za nyimbo hizi zinamwonesha baba akimiliki vyombo vya usafiri (gari) na mifugo (mbuzi):

Mfano wa 7:

**16. *Mama wa Kambo***
*Mama wa kambo…mbo*
*Mbona wanitesa…..sa*
*Sasa naondoka……ka*
*Kaa peke yako……ko*
*Koma kunipiga…...ga*
*Gari ya baba………ba*

**17. *Mbuzi***
*Mbuzi mbuzi mbuzi mbuzi wa baba*
*Mmoja katika sanduku akalia kama kasuku*
*Tisa salama mbuzi wa baba*
*Mbuzi mbuzi mbuzi mbuzi wa baba*
*Mmoja katika sanduku akalia kama kasuku*
*Nane salama mbuzi wa baba*

*Baba wa Latifa…....fa*

Hivyo, nyimbo za watoto ni mbeleko ya kusambaza majukumu ya kijinsia yaliyokumbatia utamaduni wa jamii husika kwa watoto.

## 4.2 Athari Hasi za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto

Majukumu ya kijinsia yanayopendelea jinsi moja katika nyimbo za watoto yanapandikiza mtazamo na athari hasi kwa watoto wanaozitumia. Ufafanuzi wa athari hizi umetolewa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Huweka Mipaka ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Watoto

Nyimbo za watoto zinaweka mipaka kuhusu ugawaji na utekelezaji wa majukumu kwa watoto. Majukumu ya mwanamume yaliyosawiriwa yatabaki kuwa ya mwanamume na kwa mwanamke vivyo hivyo, jambo ambalo linaleta athari kwa watoto kuona kuwa hali hiyo ni ya kawaida huku likiwasahaulisha kuwa hakuna jamii isiyopitia mabadiliko katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Utekelezaji wa majukumu mbalimbali huweza kufanywa na jinsi zote, lakini kupitia nyimbo za hizi, watoto hujifunza tofauti. Pengine nyimbo za watoto husababisha kufifisha kama si kuziua ndoto zao za kutekeleza majukumu fulani waliyojiwekea wakidhani kuwa jukumu fulani ni kwa ajili ya jinsi fulani tu na si vinginevyo. Tukirejelea data za nyimbo Na. 1, Na. 2 na Na. 3, zinamtaja mama katika jukumu la kupika hivyo ni vigumu kwa mtoto wa kiume ama mwanamume kuingia jikoni na kupika au kuwaza kwa namna tofauti. Vilevile, majukumu ya kumiliki mali (taz. data za nyimbo Na. 16 na Na. 17) na kutoa adhabu (taz. data za wimbo Na. 5) ambayo yamehusishwa na mwanamume yanamnyima mwanamke haki ya kurithi na kumiliki mali na kutoa adhabu kama mzazi. Watunzi hawana budi kuumba wahusika wa kike kwa kuwakuza ili waweze kuvuka mipaka ya jinsia na kuwa vielelezo halisi vya binadamu wanaoweza kujisimamia wenyewe; yaani wahusika hao wakuzwe ili kuwapa nafasi inayostahili katika nyaraka za kihistoria (Momanyi, 2001).

### 4.2.2 Hudumaza Fikra na Ufahamu wa Watoto

Namna majukumu yalivyogawanywa katika nyimbo za watoto huweza kudumaza fikra kwa watoto yaani kuwajengea watoto ufahamu finyu kuhusu haki zao za msingi kama vile haki ya kupata elimu ambayo ni msingi wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Tukirejea data za nyimbo, kwa mfano Na. 8 na Na. 4, mtoto wa kike ananyimwa haki yake ya msingi ya kupata elimu ilhali mtoto wa kiume anapewa fursa hiyo. Vilevile, yapo majukumu ambayo jamii imeyafanya yawe ya jinsi fulani tu na si vinginevyo. Kwa mujibu wa utafiti huu, jukumu la kupika na kulea watoto limeelekezwa kwa mwanamke na

kazi zinazodhaniwa kuwa ngumu zimepewa kibandiko cha mwanamume. Nyimbo za watoto zimemsawiri mhusika mama katika mazingira ya nyumbani akipika, akilea watoto, akichota maji na mhusika baba katika harakati za utafutaji na ndiye mwajiriwa, mmiliki na mrithi wa mali, mwenye maamuzi ya mwisho na mtoa adhabu (tazama pia Omari, 2008). Hapa ufahamu wa watoto na jamii unadumazwa kupitia mgawanyo wa majukumu katika nyimbo husika. Katika uhalisia, mwanajamii yeyote wa jinsi yoyote ana uhuru na uwezo wa kutekeleza jukumu lolote ilimradi analimudu na ana weledi wa kutosha wa kutekeleza jukumu husika.

### 4.2.3 Hufifisha Bidii na Hamasa kwa Watoto

Baadhi ya nyimbo za watoto hufifisha bidii na hamasa ya watoto na jamii katika masuala mbalimbali. Mathalani, kuhusiana na suala la elimu data ya wimbo Na. 4 inaonesha mhusika baba akiwa mstari wa mbele kwa kutaka binti yake akatishe masomo aolewe ili apate pesa ya kulipa madeni ya pombe na wakati huo huo akimwahidi mwanaye wa kiume kumlipia karo ili apate elimu. Kauli ya mhusika baba ina athari kwa bintiye ya kumfanya akose hamasa ya kwenda shule na kutofanya bidii katika masomo akijua kwamba muda wowote anaweza kukatishwa masomo. Kwa kuwa ufanisi wa kutekeleza majukumu mbalimbali hutokana na elimu, baba huyu ana malengo ya kufifisha hamasa na kuzima ndoto za bintiye za elimu alizojiwekea. Pia, katika data za wimbo Na. 8, mtoto ana masikitiko kutokana na kuona dalili za wazazi kumnyima fursa ya kupata elimu. Ingawa wimbo hauelezi ni mtoto wa jinsi ipi anayekatazwa kwenda shule, kauli ya wazazi inakatisha tamaa na hamasa kwa mtoto ikiathiri pia bidii ya masomo yake.

### 4.2.4 Huchangia Kutokujiamini kwa Watoto wa Kike

Kujiamini ni hali ya kufanya jambo kwa uhakika na bila kuwa na shaka. Ni namna nzuri ya kutekeleza majukumu kwa ufanisi na weledi wenye tija kwa ajili ya mafanikio au maendeleo yaliyokusudiwa. Kutojiamini ni kinyume cha kujiamini yaani kutokuwa na uhakika na jambo fulani linalofanyika kwa kujawa na shaka ama woga. Madhara ya kutojiamini ni pamoja na kuharibu kazi ama kusababisha hasara fulani. Pamoja na nyimbo za watoto kuwa na wahusika wengi wanawake, baadhi ya nafasi na majukumu wanayotekeleza yamejaa kejeli na dharau. Chanzo cha dharau hii ni mwanamume ambaye haoni umuhimu wa majukumu ya mwanamke na mchango wake katika ngazi ya familia, jamii na taifa. Mathalani, katika wimbo Na. 4, mhusika baba (mume) anatoa kauli za maudhi hata baada ya kuorodheshewa majukumu ya kutwa nzima aliyoyafanya mkewe. Baba huyu pia anamtolea bintiye kauli zenye kadhia kwa kumwambia aache shule na aolewe ili apate pesa ya mahari akalipe madeni ya pombe. Je, baba huyu haelewi umuhimu wa elimu kwa bintiye?

Vilevile, katika data za wimbo Na. 18 mhusika babu anatoa adhabu ya kipigo kwa mkewe bibi. Bibi analalama kuchoshwa na kazi na kipigo na anaamua kufanya mipango ya kurudi kwao. Tuangalie mfano huu:

Mfano wa 8:

**18. Bibi Kikongwe**
*Bibi kikongwe analia kwa uchungu*
*Kapigwa na babu Kikongwe*
*Kasahau kusafisha viatu*
*Anarudi kwao kwa uchungu*
*Kachoka kupigwa na kufanya kazi*

Hasira na ukali dhidi ya mwanamke na majukumu yake ni sababu za kupandikiza na kupalilia woga ambao unaathiri kujiamini kwa jinsi inayodharauliwa. Nyimbo hizi zinaacha taathira hasi kwa watoto, hususani kwa watoto wa kike, ambao watakosa kujiamini mbele ya mwanamume, jamii na taifa, watajidharau, kukata tamaa, kujiona hawana thamani, kuathirika kisaikolojia na hata kujenga chuki na uadui dhidi ya jinsi onevu.

### 4.2.5 Humpendelea Mwanamume na Mtoto wa Kiume

Kama ambavyo tumebaini, baadhi ya nyimbo za watoto zikidharau na kukejeli jinsi ya kike, nyimbo hizi zinampendelea mtoto wa kiume. Jinsi ya kiume imepewa nafasi ya upendeleo wa wazi kwa kuiona ina thamani kubwa na ni bora kuliko jinsi ya kike. Tukichunguza data za wimbo Na. 4, mume anaonekana hashiriki katika jukumu lolote la nyumbani na wakati huo huo akitaka kila jukumu litekelezwe na mkewe kwa haraka na kwa wakati. Kwa upande wa watoto, mtoto wa kike anashiriki kazi za nyumbani anapombembeleza babake atulize hasira kwa kumwahidi kumtafutia maji ya kuoga. Mtoto wa kiume haoneshwi akishiriki shughuli zozote za nyumbani. Katika wimbo huu Na. 4, upendeleo unaonekana wazi katika kuwapatia watoto elimu. Baba haoni umuhimu wa bintiye kupata elimu ilhali anamwahidi mwanawe (wa kiume) kumpeleka shuleni. Upendeleo wa elimu unapatikana pia katika nyimbo Na. 1, Na. 2 na Na.3. Katika hili serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kubaini uwiano usio sawa wa elimu kwa misingi ya jinsi, iliweka mikakati ya kuhakikisha watoto wote wanapata elimu kupitia Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (PEDEP) ambapo Sensa ya Mwaka 2012 imefanikisha ongezeko la watoto wa kike shuleni kwa uwiano wa 78% (wavulana) na 75% (wasichana).

## 5.0 Hitimisho

Katika makala haya tumechambua athari za mgawanyo tofauti wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto ambazo tumezikusanya kutoka katika mkoa

wa Dar es Salaam. Mgawanyo tofauti wa majukumu hayo umebainika kuwa na athari chanya na hasi kwa watoto wanaoziimba na hivyo bila kudhamiria hujikuta wakijifunza majukumu ya kijinsia kupitia nyimbo hizi. Athari hasi za mgawanyo tofauti wa majukumu ya kijinsia katika nyimbo za watoto, kwa mfano, kuwa na upendeleo kwa mtoto wa kiume, kufifisha bidii na hamasa, kutojiamini kwa mtoto wa kike na kudumaza fikra na ufahamu wa watoto, zina madhara zaidi kwa mtoto wa kike kuliko mtoto wa kiume. Kwa hali hii ni jukumu la wadau wote (wazazi/walezi, walimu, wanataaluma, watafiti, wanaharakati na watunzi wa fasihi ya watoto kuwa na mikakati ya pamoja ya kubadilisha mitazamo ya kijamii inayoendeleza upendeleo na ubaguzi katika utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa jinsi ya mtoto. Jukumu hili limeanza kuchomoza katika nyimbo chache za watoto zilizotungwa hivi karibuni zikijaribu kupandikiza mbegu ya usawa katika kutekeleza majukumu anuwai. Hizi ni pamoja na nyimbo zenye majukumu kama vile kufanya biashara katika wimbo (Na. 19 *Shikamoo*), kufanya kazi za shamba (Na. 20 *Mama Huyoo*) na kupata elimu (Na. 8 *Baba na Mama*, Na. 9 *Fursa* na Na. 10 *Wazazi*).

**Marejeleo**

Balisidya, M. (1987). “Tanzu za Fasihi Simulizi” katika *Mulika* Na. 19 (TUKI): 2 - 10.

Bem, S.L. (1981). “Gender Schema Theory: A Cognitive Account of Sex-typing” in *Psychological Review* (88): 354 - 364.

Berger, P.L. na Luckman, T. (1990). *The Social Construction of Reality: A Treatise in the Sociology of Knowledge*. New York: Anchor Books.

Carlson, E.A. Egeland, B. na Sroufe, A. (2004). “The Construction of Experience: A Longitudinal Study of Representation and Behaviour.” *Child Development:* 66 - 83.

Finnegan, R. (1992). *Oral Tradition and Verbal Art: A Guide to Research Practice*. London: New Fetter Lane.

Huck, C. (1979) *Children's Literature in Elementary School*. New York: Holt Rinehart and Wiston.

King'ei, K. na C.N.M. Kisovi (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Lyimo E.B. (2014) “Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau Nchini Tanzania.” Digrii ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mackinnon, C. A. (1991). *Toward A Feminist Theory of the State*. London: Harvard University Press.

Martin, C.L. na Halverson C.F. (1983). “The Effects of Sex-typing Schemas on Young Children’s Memory” in *Child Development* 54: 74 - 563.

Momanyi, C. (2001) “Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaban Robert” katika *Kiswahili* Jz. 64.(TUKI): 53 - 63.

Mnenuka, A. (2017) “Exploring Modernity in African Orature: The Bena Case Study.” PhD Dissertation, University of Leipzig, Germany.

Mrikaria, S.E. (2012). “Majukumu na Athari za Nyimbo za Watoto katika Enzi za Teknolojia ya Kidijiti: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto nchini Tanzania” katika *Mulika*31: 75 -88.

Msokile, M. (1981). “Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii Inayobadilika.” *Semina ya Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. (1975). Ushairi wa Kiswahili na Ubantu hadi 1700: Maendeleo, Mabadiliko na Uhusiano na Ubantu na Mfumo wa Jamii. Kazi Maalumu ya Mwaka wa 3. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mwanzi, H.O. (2006). “Children’s Literature: The Concept of Sociolizing the Young” in *Nairobi Journal of Literature* 4: 49 - 62.

Ndulute (1977). *The Place of Songs in Hehe Oral Literature*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
Ndumbaro, T.P. (1993). *Jifunze kwa Nyimbo: Nyimbo za Shule ya Msingi*. Dar es Salaam: Longman Tanzania Limited.
_________(1999). *Nyimbo za Watoto: Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: Universal Publications.
Omari, S. (2008). "Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania"' katika *Kiswahili*71: 98 - 107.
Ostergaad, L. (1992). *Gender and Development*. London: Routlege.
Simiyu, W.F. (2002). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza: Serengeti Book Shop.
TLS (2016). Jinsia na Ukatili wa Kijinsia: Sheria katika Lugha Rahisi. Dar es Salaam: TGNP Tanzania.
Tong, R. (1989). *Feminist Thought: A Comprehensive Introduction*. Colorado: Westview Press Inc.
Tuttle, L. (1986). *Encyclopedia of Feminism*. London: Longman.
Ussi, U. J (2015). Suala la Utendaji katika Michezo ya Jadi ya Watoto: Mifano kutoka Bumbwini Zanzibar. Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).
Weitzman, L., Eifler, D., Hokada, E., Ross, C. (1972). "Sex-Role Socialization in Picture Books for Pre school Children" in *American Journal of Sociology* 77(6): 1125-1150.